

Je niko katika hali hatari kazini?

carie | 
CENTER FOR ADJUSTMENT, RESILIENCE & RECOVERY

Mtu anapomfanya mtoto hila, kumuumiza au kumlazimisha mtoto aliye chini ya umri wa miaka 18 amfanyie kazi bila kumtendea haki au kumlipa vya kutosha, **huu ni ulanguzi wa kazi za watoto.** Inaweza kuwa katika kazi kama vile kusafisha nyumba au kufanya kazi katika mashamba, pamoja na kuomba na kuuza madawa ya kulevyia. Ni muhimu kukumbuka kwamba **haya ni makosa** na kwamba **UNA haki ya kupata msaada.**

Unaweza kuwa katika hali ya ulanguzi ikiwa:



Huna uhakika ni lini na jinsi gani huwa unalipwa



Huruhusiwi kuunganika na familia



Huruhusiwi kwenda shuleni



Unatarajiwa kuhudumia wengine hata wakati hutaki



Mtu atachukua hati zako muhimu kama vile pasipoti au kitambulisho chako



Wewe na wengine **mliumia mkifanya kazi** na hamkuruhusiwa kumuona daktari



Unaishi **palepale** unapofanya kazi



Familia yako katika nchi yako ya nyumbani **inatishiwa**



Ni wewe pekee **unayetunza wadogo wako**



Mtu anaahidi **atalipa deni lako** ikiwa utamfanya kazi



Unawajibika **kifedha kwa familia yako**



Unatishiwa **kupelekwa kwa idara ya uhamiaji** au kufukuzwa nchini



Ikiwa wewe au mtu unayemjua anapitia haya, kuna msaada!

Piga simu kwa 911 ikiwa uko katika hatari ya haraka. National Human Trafficking Hotline (Nambari ya Simu ya Kitaifa ya Ulanguzi wa Binadamu) husaidia, **saa 24 kwa siku, siku 7 kwa wiki** kwa kupiga 1-888-373-7888 na usaidizi katika **lughu zaidi ya 200.**